## Somo la 1: Utangulizi


**Je, vifaa saidizi vya kupangilia dawa ni nini na ni nani anayevitumia?**

Vifaa saidizi vya kupangilia umezaji wa dawa vinasaidia watu:

- Kupangilia dawa kwa kadri walivyoshauriwa na daktari.
- Kujitegemea na kupunguza utegemezi kwa watu wanaotoa msaada wa kuwatunza
- Kuepuka kusahau au kumeza dawa nyingi kuliko kipimo.
- Kutokuhitaji kufungua na kufunga pakiti nyingi za dawa kila siku.

**Sifa za vifaa saidizi vya kupangilia umezaji wa dawa**

Vifaa saidizi vya kupangilia umezaji dawa vinaweza kuwa na sehemu moja au sehemu nyingi ya kuweka dawa za kila siku ya juma.

| **Kifaa saidizi chenye sehemu moja ya kupangilia umezaji dawa** | **Kifaa saidizi chenye sehemu nyingi za kupangilia umezaji dawa** |
|---|---|
|   |  |

| **Sifa muhimu** | **Sifa za ziada** |
|---|---|
| ✓ Kifaa saidizi ambacho kinapitisha mwanga kumwezesha mtu kuona ndani<br>✓ Kina uzito mwepesi<br>✓ Kina alama zinazoonyesha kila siku ya Juma<br>✓ Kina kifuniko kwa kila sehemu ya kuweka dawa. | • Alama za brele<br>• Ina rangi tofauti<br>• Ina vifuniko vinavyoweza kubanwa |

Mgonjwa anaweza kuhitaji kifaa saidizi cha kupangilia umezaji dawa iwapo anapata taabu ya kupangilia na kutunza dawa zake na/au kukumbuka kumeza kila dawa. Msaidizi wa mgonjwa anaweza kufaidika na matumizi ya kifaa saidizi cha kupangilia dawa ili kumsaidia mgonjwa ambaye anapata taabu kumeza dawa zake.

**Kama mgonjwa anasahau kumeza dawa zake au anameza dawa zaidi kwa bahati mbaya yote haya mawili yanaweza kuhatarisha afya yake.**

## Somo la 2: Hatua ya 1: Kuchagua

**Tathimini**

Hatua ya kwanza ya kugawa kifaa saidizi cha kupangilia umezaji dawa ni kutathmini mahitaji ya mgonjwa na kuchagua kifaa kinachomfaa zaidi. Kama mtu anahitaji msaada wa kumeza dawa, ni muhimu kuangalia kama msaidizi yupo ili kumsaidia kuweza kumeza dawa.  Kama msaidizi hayupo ☞mpe rufaa kwenda kwa daktari au mfamasia.

**Orodha ya dawa**

Kwa kushirikiana na mgonjwa, jaza orodha yote ya dawa **zote** ambazo mgonjwa anameza. Taarifa hii itatumika kumsaidia mgonjwa kuweka dawa zake kwenye kifaa saidizi kwa usahihi.

Kama mgonjwa amepata madhara kutokana na umezaji dawa kwa wakati uliopita, toa maelezo. Hii itamsaidia mfamasia au daktari kutokumpa dawa hizo ambazo mgonjwa ana mzio (aleji) nazo.

Orodha ya dawa inapaswa kufanyiwa mapitio kila baada ya miezi 6-12 au muda mfupi zaidi, kama mgonjwa amebadilishwa dawa zake

Mgonjwa anapaswa kujua wakati wa kusitisha au kubadilisha dawa.

| **Jambo** | **Sababu** |
|---|---|
| Elezea muoekano wa kidonge | Rangi, umbo, alama, ukubwa. Kuchora kuzunguka kidonge kunaweza kusaidia. |
| Andika ugonjwa unaotibiwa na dawa | Tumia lugha rahisi inayoeleweka |
| Andika dozi na idadi ya vidonge | Kokotoa idadi ya vidonge ambavyo mgonjwa anapaswa kumeza ili kufikia dozi iliyoshauriwa |
| Andika jina la daktari aliyeshauri dawa | Inasadia kujua aliyeandika dawa kama mgonjwa au msaidizi wake ana swali lolote. |
| Andika idadi ya umezaji dawa kwa siku, ambayo mgonjwa anapaswa kuzingatia. | Idadi za umezaji dawa zitaonyesha aina ya kifaa saidizi kinachomfaa mgonjwa zaidi |
| Andika kama kuna maelekezo maalum. | Taarifa yoyote kuhusu namna na wakati wa kumeza dawa |

Toa rufaa kwa mgonjwa kwenda kwa daktari au Mfamasia kama kuna taarifa inakosekana au haieleweki.

## Somo la 3: Hatua ya pili: Kutumia

**Kufundisha kuhusu namna y a kumeza dawa.**

Hatua ya pili katika ugawaji wa kifaa saidizi cha kupangilia umezaji dawa ni kumfundisha mgonjwa namna ya kutumia na kutunza kifaa hiki. Mueleze kwamba kifaa saidizi hiki kitamsaidia kupangilia dawa zake atakazo zimeza kwa juma zima. Kitamsaidia kuharikisha na kumrahisishia kumeza dawa zake kila siku. Kitarahisisha kujua kama dozi za dawa zimemezwa au zimesahaulika.

Mhamasishe kumhusisha mtu anayemtunza. Jicho lingine litaepusha makosa wakati wa kuweka dawa kwenye kifaa saidizi hiki.

Kabla ya kumuonyesha mgonjwa namna ya kuweka dawa kwenye kifaa saidizi cha kupangilia dawa, kagua tarehe zilizoko kwenye orodha yake ya dawa na muulize kama kuna mabadiliko yoyote. Boresha orodha kama inatakiwa.

- Waonyeshe namna ya kutambua kila kila kidonge na
- Weka dawa kwene kifaa saidizi kulingana na orodha ya dawa.
- Mfundishe mgonjwa namna ya kuweka dawa moja baada ya nyingine.
- Weka dawa kwenye kifaa saidizi cha kupangilia umezaji dawa kwa juma zima.

Jadili na mgonjwa kuhusu umezaji dawa wa kila siku. Utaratibu huu utamsaidia kukumbuka kumeza dawa.

Kumbuka kuangalia maelekezo maalum wakati wa kupanga umezaji dawa.

Ili kusafisha kifaa saidizi cha kupangilia dawa, toa dawa zote na kioshe kwa maji ya uvuguvugu na sabuni. Kikaushe na kitambaa laini kabla ya kuweka dawa.

## Somo la 4: Hatua ya tatu: Ufuatiliaji

### Kazi za ufuatiliaji

Hakikisha kuwa kifaa saidizi bado kinakidhi majhitaji ya mgonjwa na kiko katika hali nzuri ya kufanya kazi. Fuatilia ndani ya mwezi mmoja watu wote ambao wanaweza kutumia vifaa saidizi vya kupangilia umezaji dawa.

Kama mgonjwa hatumii kifaa saidizi cha kupangilia umezaji dawa au ana matatizo, muulize ili ujue sababu. Aidha kwa kushirikiana na mgonjwa mnaweza kutafuta jawabu kwa pamoja na kumpa rufaa kwenda kwa daktari.

Mhamasishe mgonjwa kumuomba daktari au Mfamasia wake kupitia orodha ya dawa zake kila baada ya miezi 6-12. Wanaweza kuhitaji kufanyiwa tathmini kila mara kama maradhi ya mgonjwa yanabadilika kila mara.